# Wakulima wakabidhiwa vipande 700,000 vya kamba za manila

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah amekabidhi vipande vya kamba za manila 700,000 kwa wakulima wa mwani katika Kijiji cha Songosongo, wilayani Kilwa, mkoa wa Lindi.

Akizungumza na wananchi wa Songosongo juzi Dkt. Tamatamah alisema Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) imetoa kamba hizi ili kuwawezesha wakulima wa mwani, kwani kamba ilikuwa ni moja ya changamoto waliyokuwa wakikabiliana nayo.

Kamba hizi za manila (ambazo kila moja ina urefu wa mita 10) katika kilimo cha mwani, hufungwa katika vigingi na hutumika kwa ajili ya kuoteshea mwani ambapo mwani hufungwa katika kamba hizo zinazosaidia pia mwani kutochukuliwa na maji ya bahari pale panapokuwepo na wimbi.

Dkt. Tamatamah alisema duniani kote kwa sasa mwani unalimwa kibiashara, hivyo mwani ni moja ya zao linalopewa kipaumbele katika wizara. Katika kilimo cha mwani wakulima wanakutana na changamoto mbalimbali zikiwemo za ukosefu wa mitaji na masoko.

"Wizara kupitia sekta ya uvuvi imeanza kutoa kamba ambazo ni moja ya pembejeo muhimu kwa wakulima wa mwani ikiwa ni sehemu ya kuwawezesha wakulima hao kwa kuwapunguzia sehemu ya gharama za uzalishaji ili baadae waweze kusimama wenyewe," alisema Dkt. Tamatamah.

Pia alisema kuwa kama wakulima watalima vizuri katika kamba moja ya mita kumi katika bamvua nne (miezi miwili) wanaweza kupata kati ya kilo 8-10, na kamba hizo walizopewa zinaweza kutumika kwa mwaka mzima. Lengo la wizara ni kusambaza kamba hizi kwa wakulima wa mwani maeneo yote Tanzania Bara.

Dkt. Tamatamah alisema kuwa ipo changamoto ya soko la mwani hasa kwenye bei, kwani kwa sasa asilimia 90 ya mwani inauzwa nje ikiwa ghafi na ni asilimia 10 tu ndio inayotumika hapa nchini.

Hivyo wizara kwa sasa inawahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi na kuwaunganisha na taasisi za kifedha ili waweze kukopesheka na waweze kuanzisha viwanda vidogo vya kuchakata mwani ili kuongeza thamani.

Hii itasaidia kupunguza kiasi cha asilimia ya mwani inayokwenda nje ya nchi ikiwa ghafi na kusaidia kuongeza ajira. Aidha, Katibu Mkuu Tamatamah alisema zao la mwani linazo faida kubwa ikiwa ni pamoja na kuongeza kipato katika jamii za maeneo ya pwani hasa kwa akina mama, inaondoa umaskini lakini pia linaingiza fedha za kigeni.

Naye mkulima wa mwani, Mbimbisa Omary alimshukuru Katibu Mkuu Tamatamah kwa kuwaletea vitendea kazi kwa ajili ya kilimo cha mwani. Mbimbisa alisema kilimo cha mwani kinawasaidia mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuwasomesha Watoto, kununua chakula pamoja na ujenzi wa nyumba.

Jaka Farahani ambaye ni mkulima wa mwani alisema changamoto ya masoko inawasumbua sana hasa pale wanunuzi wanaowategemea wasiponunua hivyo ameiomba wizara kuwasaidia kutatua changamoto hiyo. Lakini pia amemuomba Katibu Mkuu kuendelea kuwapelekea kamba nyingi zaidi kwa kuwa eneo la kulima ni kubwa na wakulima wapo wengi.

Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji (WMUV), Dkt. Nazael Madalla alisema wizara kupitia idara yake inaendelea kuhamasisha kampuni kuendelea kuchukua leseni kwa ajili ya kununua mwani na mpaka sasa zipo kampuni 7.

Lengo la kuwa na kampuni nyingi ni kuongeza ushindani hivyo kampuni zinahamasishwa kujisajili ili zitambulike na ziweze kufanya biashara ya mwani. Zao la mwani hapa nchini Tanzania lilianza kulimwa miaka ya 1980 na lilianzishwa katika kisiwa cha Zanzibar.

Baada ya kufanikiwa katika kipindi cha majaribio, miaka ya 1990 mpaka 2000 Tanzania hususani Zanzibar ilikuwa ni nchi ya kwanza duniani kwa uzalishaji wa mwani. Lakini kutokana na changamoto mbalimbali kwa sasa Tanzania ni nchi ya tatu kwa uzalishaji wa mwani ambapo nchi ya kwanza ni Ufilipino ikifuatwa na Indonesia.



Scanned with CamScanner



**USHIRIKIANO: Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Air Tanzania, Edward Nkwabi na Mkurugenzi wa Airtel Tanzania, Isaack Nchunda wakipongezana baada ya uzinduzi wa ushirikiano na Airtel Tanzania ambapo kuanzia sasa, wateja wao wataweza kununua tiketi za kusafiri kwa Air Tanzania kupitia akaunti zao za Airtel Money.**

# Dk. Tamatamah akabidhi kamba 700,000 kwa wakulima wa mwani

**Na MWANDISHI WETU**

**-KILWA**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk Rashid Tamatamah amekabidhi vipande vya kamba za mamila 700,000 kwa wakulima wa mwani Kijiji cha Songosongo wilayani Kilwa, mkoa wa Lindi.

Akizungumza na wananchi wa Songosongo jana, Dk. Tamatamah alisema Serikali imetoa kamba hizo ili kuwawezesha wakulima wa mwani kwani kamba ilikuwa ni moja ya changamoto waliyokuwa wakikabiliana nayo.

Kamba hizo kila moja ina urefu wa mita 10 katika kilimo cha mwani, hufungwa katika vigingi na hutumika kwa ajili ya kuoteshea mwani ambapo mwani hufungwa katika kamba hizo zinazosaidia pia mwani kutochukuliwa na maji ya bahari pale panapokuwepo na wimbi.

Alisema duniani kote kwa sasa mwani unalimwa kibiashara, ni moja ya zao linalopewa kipaumbele katika wizara. Katika kilimo cha mwani wakulima wanakutana na changamoto mbalimbali zikiwemo za ukosefu wa mitaji na masoko.

Alisema kama wakulima watalima vizuri katika kamba moja ya mita kumi katika kamvua nne, wanaweza kupata kati ya kilo 8-10 na kamba zinaweza kutumika mwaka mzima. Lengo la wizara ni kusambaza kamba hizi kwa wakulima maeneo yote.

Alisema ipo changamoto ya soko la mwani hasa kwenye bei kwani kwa sasa asilimia 90 ya mwani inauzwa nje, ikiwa ghafi na ni asilimia 10 tu ndio inayotumika hapa nchini.

Mkulima wa mwani, Mbimbisa Omary alisema kilimo kinawasaidia mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuwasomesha Watoto, kununua chakula pamoja na ujenzi wa nyumba.

Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji (WMUV), Dk. Nazael Madalla alisema wizara kupitia idara yake inaendelea kuhamasisha kampuni kuendelea kuchukua leseni kwa ajili ya kununua mwani na mpaka sasa zipo kampuni 7. Lengo la kuwa na kampuni nyingi ni kuongeza ushindani hivyo kampuni zinahamasishwa kujisajili ili zitambulike na ziweze kufanya biashara ya mwani.

Scanned with CamScanner

# Wakulima wa mwani Kilwa wapigwa jeki

**Na Mwandishi Maalumu, Kilwa**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk Rashid Tamatamah (pichani) amekabidhi vipande vya kamba za marula 700,000 kwa wakulima wa mwani katika kijiji cha Songosongo, wilayani Kilwa, mkoa wa Lindi.



Akizungumza na wananchi wa Songosongo jana, Dk Tamatamah alisema wizara hiyo imetoa kamba hizo ili kuwawezesha wakulima wa zao hilo kutokana na changamoto inayowakabili ya kutokuwa na kamba hizo.

Kamba hizo ambazo kila moja ina urefu wa mita 10, zitatumika kufungwa katika vigingi kwa ajili ya kuoteshea mwani.

Kamba hizo zinasaidia mwani kutochukuliwa na maji ya bahari panapokuwapo na mawimbi.

Dk Tamatamah alisema duniani kote kwa sasa mwani unalimwa kibiashara, hivyo ni moja ya mazao yanayopewa kipaumbele na wizara hiyo.

"Wizara kupitia sekta ya uvuvi imeanza kutoa kamba ambazo ni moja ya pembejeo muhimu kwa wakulima wa mwani, ikiwa ni sehemu ya kuwawezesha wakulima hao kwa kuwapunguzia sehemu ya gharama za uzalishaji waweze kusimama wenyewe," alisema.

Alisema kama wakulima hao watalima vizuri, kamba moja ya mita 10 katika bamvua nne (miezi miwili) wanaweza kupata mavuno kati ya kilo nane hadi 10 na zinaweza kutumika kwa mwaka mzima.

"Lengo la wizara ni kusambaza kamba hizo kwa wakulima wa mwani maeneo yote Tanzania Bara," alisema.

Hata hivyo, Katibu Mkuu huyo alisema ipo changamoto ya soko la mwani hasa kwenye bei kwani kwa sasa asilimia 90 ya inauzwa nje ikiwa ghafi na ni asilimia 10 tu ndio inayotumika nchini.

Alisema wizara hiyo inawahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi na kuwaunganisha na taasisi za fedha ili wakopesheka na waanzishe viwanda vidogo vya kuchakata mwani kuongeza thamani.

Mkulima wa mwani, Mbimbisa Omary alisema kilimo hicho kinawasaidia mambo mengi ikiwamo kuwasomesha watoto, kununua chakula na ujenzi wa nyumba.

Mkulima mwingine, Jaka Farahani alisema changamoto inayowasumbua ni soko na kuiomba wizara kuwasaidia kutatua changamoto hiyo.

Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji (WMUV), Dk Nazael Madalla alisema wizara kupitia idara hiyo inaendelea kuhamasisha kampuni kuendelea kuchukua leseni za kununua mwani na mpaka sasa kampuni saba zimejitokeza.

Alisema lengo la kuwa na kampuni nyingi ni kuongeza ushindani katika biashara ya mwani.

Zao la mwani nchini lilianza kulimwa miaka ya 1980 na lilianzishwa Zanzibar.

Baada ya kufanikiwa katika kipindi cha majaribio, miaka ya 1990 mpaka 2000 Tanzania hususani Zanzibar ilikuwa ni nchi ya kwanza duniani kwa uzalishaji wa zao hilo, lakini kutokana na changamoto mbalimbali kwa sasa ni ya tatu ikitanguliwa na Ufilipino na Indonesia.


**CHETI KIMEPOTEA**



**KULWA JOHN BATULE**

Anatangaza kupotelewa na cheti cha Kidato cha Sita KWIRO SECONDARY SCHOOL, index No. S 0123-0652 cha mwaka 2013. Yeyote atakayekiona, anaombwa kukoa taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

CHETI KIMEPOTEA


Scanned with CamScanner

hizo zinazosaidia pia mwani kutochukuliwa na maji ya bahari pale panapokuwepo na wimbi.

Dkt. Tamatamah alisema duniani kote kwa sasa mwani unalimwa kibiashara, hivyo mwani ni moja ya zao linalopewa kipaumbele katika wizara. Katika kilimo cha

ipo changamoto ya soko la mwani hasa kwenye bei, kwani kwa sasa asilimia 90 ya mwani inauzwa nje ikiwa ghafi na ni asilimia 10 tu ndio inayotumika hapa nchini.

Hivyo wizara kwa sasa inawahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi na kuwaunganisha

na ujenzi wa nyumba.

Jaka Farahani ambaye ni mkulima wa mwani alisema changamoto ya masoko inawasumbua sana hasa pale wanunuzi wanaowategemea wasiponunua hivyo ameiomba wizara kuwasaidia kutatua changamoto hiyo. Lakini pia

cha majaribio, miaka ya 1990 mpaka 2000 Tanzania hususani Zanzibar ilikuwa ni nchi ya kwanza duniani kwa uzalishaji wa mwani. Lakini kutokana na changamoto mbalimbali kwa sasa Tanzania ni nchi ya tatu kwa uzalishaji wa mwani ambapo nchi ya kwanza ni Ufilipino ikifuatiwa na Indonesia.



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt Rashid Tamatamah, akikabidhi kamba kwa ajili ya wakulima wa mwani kwa Mwenyekiti Kijiji cha Songosongo wilayani Kilwa, Swaluya Sadi (kushoto), juzi, ambako alikabidhi kamba hizo jumla 700,000. Katikati ni Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbemaji (WMUV), Dkt. Nazael Madalla.** (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner